# Usawiri wa Nduni za Shujaa na Nafasi yake katika kuibua Maudhui: Ukakiki wa Kisakale cha "Mukwavinyika"

*Aneth Kasebele*
*Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa*

**Ikisiri**

**Mjadala wa kuwapo au kutokuwapo kwa mashujaa wa Kiafrika ulichochewa na Finnegan (1970) aliposema kuwa Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara hakuna tendi zinazozungumzia habari za mashujaa. Kutokana na hilo, watafiti wa Kiafrika kama vile Johnson (1978), Okpewho (1979), na Mulokozi (1999) walifanya tafiti ili kumjibu Finnegan. Matokeo ya tafiti zao yamedhihirisha kuwa, Afrika kuna tendi zinazozungumzia habari za mashujaa na ushujaa. Pia, kumhusu shujaa wa Kiafrika, watafiti hao waliorodhesha sifa kadhaa anazotakiwa kuwa nazo shujaa wa Kiafrika. Sifa hizo ni shujaa kutoka katika tabaka lolote, kusaidiwa na wahenga au mizimu, kuungwa mkono na wanajamii, kuongozwa na sihiri na kuwa na nguvu zinazojumuisha nguvu za kimwili, kiakili, kivita na urijali. Hata hivyo, imezoeleka kwa watafiti wengi kuwa mashujaa wanachambuliwa kwa kutumia utanzu wa utendi (Mtega, 2017; Kazinja, 2017 na Mulokozi, 2017). Hili, zaidi ya mengine, limesababisha hata mashujaa hao kujulikana kuwa ni mashujaa wa kiutendi. Pia, kumekuwa na tafiti chache kuhusu uchambuzi wa mashujaa wa Kiafrika kwa kutumia tanzu nyingine za fasihi kama vile visakale. Kwa kutambua hoja hiyo, makala hii inakusudia kuchunguza nduni za shujaa na nafasi yake katika kuibua maudhui huku ikidondoa mifano kutoka katika kisakale cha "Mukwavinyika." Makala hii, imeongozwa na Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika na data zake zimekusanywa maktabani na uwandani. Makala hii, imebainisha kuwa, sifa za shujaa zina mchango mkubwa katika kuibua maudhui yanayosawiriwa katika visakale vya mashujaa wa jamii husika.**

**Maneno Muhimu**: Shujaa, Maudhui, Kisakale, Usawiri

## Utangulizi

Mashujaa wa Kiafrika wamekuwa wakisawiriwa katika tanzu mbalimbali za fasihi simulizi na andishi za jamii zao. Miongoni mwa tanzu hizo ni utendi, nyimbo, ngano, visakale, riwaya na tamthiliya. Makala hii imechunguza usawiri wa sifa za shujaa kwa kutumia utanzu wa visakale. Kutokana na hilo, utafiti huu una mchango mkubwa sana katika kuonesha ufungamano uliopo baina ya visakale na mashujaa.

Visakale ni masimulizi ya kimapokeo juu ya wahenga, mashujaa au watu maarufu walioishi katika jamii yenye kuchanganya chuku na historia halisi (Ngure, 2003; Samwel, 2012; Mulokozi, 2017 na Mlaga, 2017). Akifafanua mawazo hayo, Ngure (2003) anaeleza kuwa visakale ni usimulizi unaomzungukia mhusika wa kihistoria au matukio na mara nyingi wahusika wake huwa na uwezo wa kiungu unaowawezesha kutenda matendo ya uki-Maumbile. Ngure anaendelea kufafanua kuwa mara nyingi visakale vikisimuliwa kwa muda mrefu huwa vinatiwa chuku nyingi mno kiasi cha kutoweza kuaminika. Naye, Mulokozi (2017) anaeleza kuwa visakale ni masimulizi ya kimapokeo kuhusu wahenga au mashujaa wa kabila au taifa yenye kuchanganya chuku na historia halisi. Mulokozi anaeleza zaidi kwamba mara nyingi visakale huwa vinahusu watu muhimu waliofanya au wanaaminiwa kuwa walifanya mambo makubwa katika jamii zao. Anawataja hawa kuwa ni pamoja na waanzilishi wa ukoo, kabila au taifa, waanzilishi wa madhehebu ya dini, mashujaa wa vita au ulinzi wa jamii, watemi na wafalme.

Hivyo basi, mara nyingi visakale vinatumia chuku kusifia matendo na uwezo wa shujaa ambaye aliishi katika jamii. Pia, visakale vinahifadhi historia halisi ya mhusika kiasi kwamba wanajamii wanaziamini kuwa ni hadithi zihusuzo matukio ya kweli yaliyopata kutokea katika jamii. Katika jamii za Kiafrika kuna masimulizi mengi ya mashujaa ambao habari zao zimechanganywa na visakale kama vile, Sunjata, Shaka, Kinjeketile, Ng'wanamalundi, Mukwavinyika[1], Mirambo na Nyerere. Kutokana na hayo, makala hii ina lengo la kufafanua usawiri wa nduni[2] za shujaa na nafasi yake katika kuibua maudhui. Ili kufikiwa kwa lengo hilo, makala hii," imegawanywa katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi; sehemu ya pili inaeleza muhtasari wa kisakale cha "Mukwavinyika"; sehemu ya tatu inafafanua nadharia iliyoongoza utafiti huu; sehemu ya nne inafafanua jinsi nduni za shujaa zilivyoibua maudhui katika kisakale husika na sehemu ya tano ni hitimisho.

**Muhtasari wa Kisakale cha Mukwavinyika**

Kisakale cha "Mukwavinyika" kinamhusu shujaa huyo ambaye alikuwa ni mtoto wa mtawala wa jamii ya Wahehe aitwaye Munyigumba. Mukwavinyika alikabidhiwa utawala katika jamii ya Wahehe tangu akiwa kijana mdogo baada ya baba yake mzazi kufariki. Mukwavinyika alikuwa mtawala aliyependwa sana na watu wake kutokana na kuwawezesha kuwashinda maadui zao. Aidha, kila

[1] Mukwavinyika ni jina la heshima likimaanisha kiongozi aliyetwaa nchi nyingi. Jina hili alipewa na baba yake baada ya kufanikiwa kumuokoa kutoka katika vita na Wangoni. Mukwavinyika kwa sasa anafahamika pia kwa jina la Mkwawa ambalo lilifupishwa na Wajerumani wakati wa utawala wa Wajerumani huku wakilitamka Mukwava

[2] TUKI (2004) wanafasili nduni[2] kuwa ni sifa maalumu ya kitu. Hivyo, katika makala hii dhana "nduni" na "sifa" zitatumika kwa mbadilishano kurejelea kitu kilekile.

walipojitokeza maadui kupambana naye, wanajamii walijitokeza kwa wingi kumsaidia katika jeshi lake. Vilevile, baba yake Munyigumba aliendelea kumlinda na kumpigania Mkwawa hata kama alikuwa ameshafariki. Kwa mfano, wakati mmoja, Mwambambe alifanya mapinduzi na akachukua madaraka kinguvu kisha akaunda mpango mzima wa kumuua Mukwavinyika. Kutokana na hayo aliyoyafanya Mwambambe, Mukwavinyika aliona ni bora kutoroka na kwenda kuishi Ugogoni kuliko kubaki Uheheni ambako alikuwa ana hofu ya kifo.

Hata hivyo, huko Uheheni, Wahehe waliupinga utawala wa Mwambambe kwa sababu ulikuwa ni utawala wa kikatili sana. Hivyo, Wahehe walifanya shauri la siri wakamuita Mukwavinyika aje kupigana vita na Mwambambe kwa lengo la kumtoa Mwambambe madarakani. Vita kati ya Mwambambe na Mukwavinyika ilikuwa ni vita kali sana kwa sababu Mwambambe alikuwa ni mtu mwenye nguvu za ajabu. Kila wakimtupia Mwambambe mikuki mwilini ilikuwa inamchoma lakini hafi badala yake anaichomoa na kuwatupia jeshi la Mukwavinyika na alikuwa anaua watu zaidi ya kumi kwa wakati mmoja.

Usiku mmoja, Mkwawa alipokuwa amelala, alitembelewa na baba yake katika ndoto ambaye alimweleza mbinu za kutumia ili kumuua Mwambambe. Alimweleza kwamba, ili Mwambambe afe anatakiwa kuchomwa mkuki katika kisigino na kwenye dole gumba. Baada ya kuijua mbinu hiyo mfuasi wa Mkwawa ambaye ni Mkimayena alimchoma mkuki Mwambambe kama ilivyoelekezwa. Baada ya kuchomwa mkuki, Mwambambe alianza kuhisi kichefuchefu na akaanguka puu chini kama gunia kisha akakata roho. Wafuasi wa Mukwavinyika walipoona Mwambambe amekufa walimkatakata vipandevipande na kumla nyama palepale huku ikiwa mbichi.

Kisakale cha “Mukwavinyika” kinaeleza pia kuwa, Mkwawa alikuwa kiongozi tajiri na mwenye wake wengi sana waliofika sitini na mbili. Kutokana na hilo, Mkwawa alikuwa na watoto wengi sana. Shujaa huyo kila alipomwona mwanamke mzuri alimchukua kuwa mkewe na kwamba wanawake hao hawakuruhusiwa kuwa na wanaume wengine. Ili kuhakikisha kuwa wanawake wake hawaendi nje ya ndoa, Mkwawa alikuwa na nguvu za kiganga zilizomsaidia kutambua mwanamke aliyeenda nje ya ndoa na hivyo kumchukulia hatua. Kutokana na hilo, wake zake walijitahidi sana kuwa waaminifu. Vilevile Mkwawa aliogopeka sana kwa watu wake kutokana na kuwa na nguvu nyingi za kiganga ambazo zilimwezesha si tu kushinda vita bali pia kuwabaini maadui zake katika utawala wake. Hili lilimsaidia Mkwawa kudumu katika utawala wa jamii ya Wahehe.

Kisakale hicho kinaeleza kuwa utawala wa Mukwavinyika ulikuwa ni utawala wenye nguvu kwa sababu Mukwavinyika alipanua utawala wake katika eneo kubwa mpaka nje ya mipaka ya Uhehe. Pia, Mukwavinyika aliimarisha utawala wake kwa kujenga ngome kubwa katika kijiji cha Kalenga kilichopo ndani ya wilaya ya Iringa vijijini. Baada ya Mukwavinyika kuweka makazi yake rasmi katika kijiji cha Kalenga, Kalenga ilikua na kupata sifa. Waarabu walikuwa wanakuja Kalenga kwa Mukwavinyika kwa ajili ya kufanya naye biashara. Biashara kati ya Waarabu na

Mukwavinyika ilikuwa na manufaa kwa sababu ilimwezesha Mukwavinyika kununua silaha mbalimbali kama vile bunduki, fataki na baruti ambazo alizitunza katika ngome yake.

Kisakale hicho, kinaeleza kuwa katika kipindi ambacho Mukwavinyika alikuwa anaimarisha ngome yake Wajerumani walikuwa wamekwishaingia Tanganyika wakiwa wanapanua utawala wao. Wajerumani walikuwa na mashaka na Mukwavinyika kwa sababu walishasikia kuwa ni mfalme mwenye nguvu na hodari katika vita. Hivyo, Wajerumani walikwenda Kalenga kumtembelea Mukwavinyika kwa lengo la kufahamiana naye. Hata hivyo, Mukwavinyika aliwapa zawadi tu na hakuwa tayari kujadiliana nao. Wajerumani nao walipokea zawadi za Mukwavinyika bila ya wao kutoa zawadi kwake kama shukrani. Kitendo hicho cha Wajerumani kutotoa shukurani kwa Mukwavinyika kilimchukiza Mukwavinyika na kuingia katika mgogoro nao. Hivyo, mara kwa mara, Mukwavinyika na Wajerumani waliingia vitani. Katika vita vya kwanza, Mukwavinyika alishinda kwa kuwaua askari wengi wa Kijerumani huko Lugalo. Hata hivyo, katika vita vya mara ya pili, Mukwavinyika alishindwa, akazidiwa nguvu na akakimbia kwenda kujificha katika pango huko Mulambalasi. Mukwavinyika alipokuwa huko Mulambalasi alijiua kwa kujipiga risasi ili asikamatwe na Wajerumani. Hata hivyo, Wajerumani walipofika mahali ambapo Mkwawa alijificha walikuta Mkwawa ameshafariki kwa kujipiga risasi. Hivyo basi, Wajerumani waliamua kukata kichwa cha Mukwavinyika kwa ajili ya kwenda kumuonesha kiongozi wao.

**Nadharia ya Utafiti**

Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika imetokana na mawazo ya Mulokozi (2017) yaliyoasisi kile alichokiita Nadharia ya Sifa za Shujaa ambapo alipendekeza itumike kuchambua tendi za Kiafrika kwa sababu zinafungamana na mashujaa. Hata hivyo, msingi wa mawazo ya nadharia hii tumeyatumia katika kuhakiki visakale kwa sababu navyo vinafungamana na mashujaa. Madai ya msingi ya nadharia hiyo ni kuwa shujaa wa Kiafrika, bila kujali jamii atokayo, ana nduni mbalimbali. Hii, ina maana kuwa, kwa mujibu wa nadharia hii, mashujaa wa Kiafrika wana nduni zinazofanana. Miongoni mwa sifa zinazotajwa ni pamoja na shujaa wa Kiafrika kutoka katika tabaka la juu au la kawaida; shujaa kuwa na nguvu zinazojumuisha nguvu za kivita, kiakili, kimwili, na urijali, na; shujaa kuwa na sihiri. Sifa nyingine za shujaa wa Kiafrika kwa mujibu wa nadharia hii ni shujaa kusaidiwa na nguvu ya wahenga au mizimu, na; shujaa kuwa na mshikamano na watu. Kwa kutumia nadharia hii tumeweza kubaini jinsi sifa hizo zinavyojibainisha kwa Mukwavinyika.

**Nduni za Shujaa Zilivyoibua Maudhui katika Kisakale cha "Mukwavinyika"**

Kuna uhusiano wa karibu kati ya nduni za shujaa na maudhui yaliyosawiriwa katika kisakale cha "Mukwavinyika." Miongoni mwa maudhui hayo ni dhamira mbalimbali, motifu na falsafa. Maudhui hayo yamefafanuliwa kama ifuatavyo:

**Dhamira**

Dhamira mbalimbali zimeibuliwa kupitia usawiri wa nduni za shujaa katika kisakale cha "Mukwavinyika." Miongoni mwa dhamira hizo ni dhamira ya uzalendo na ukombozi, umoja na mshikamano, imani za uchawi na ushirikina, uzazi, kifo, imani juu ya wahenga na mahoka, matabaka, usaliti na nafasi ya mwanamke katika jamii. Dhamira hizo zimefafanuliwa ifuatavyo:

**Uzalendo na Ukombozi**

Dhamira hii imeibuliwa na sifa ya shujaa kuwa na nguvu za kivita. Mawazo ya wafuasi wa Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika yanasema kuwa, shujaa wa Kiafrika ni lazima apigane vita (Kazinja, 2017 na Mulokozi, 2017). Katika kisakale cha "Mukwavinyika" imebainika kuwa Mukwavinyika alipigana vita na maadui kwa ajili ya kuitetea jamii yake. Kitendo cha Mukwavinyika kupigana vita kinaonesha jinsi shujaa huyu alivyo mzalendo na jinsi alivyoikomboa jamii yake. Katika kisakale hicho, imeelezwa kwamba Mukwavinyika kwa mara ya kwanza alipigana vita na Wangoni ambao walivamia jamii ya Wahehe. Katika vita hiyo Mukwavinyika alishinda kwa kuwafukuza Wangoni kutoka kwa jamii ya Wahehe. Katika data namba (1) hayo yamejidhihrisha kama ifuatavyo:

(1) ...Mukwavinyika alipokuwa kijana mdogo alifanya maajabu, na hasa katika ufundi wa kupigana vita. Loooh! watu walishangaa haaaaaaa! kumbeeee! kijana huyu anaweza kupigana vita kiasi hiki. Katika vita hivyo, Mukwavinyika aliwafukuza Wangoni kama mtu amfukuzavyo mwizi...

Maelezo katika dondoo namba (1) yanaonyesha jinsi Mukwavinyika alivyopigana vita na wangoni. Wangoni ni moja ya makabila yanayotajwa kuwa na nguvu nyingi za kivita. Jamii hiyo inatajwa kuwa tishio toka zama za vita vya Mfecane vilivyowaleta Wangoni Tanzania kutokea Afrika ya Kusini. Wangoni walikuwa na mbinu za kisasa za kivita zilizowafanya waweze kuziteka jamii nyingine. Hata hivyo, mbali na nguvu hizi za kivita, uhodari na mbinu za kisasa za kivita, Wangoni walishindwa vibaya katika vita vyao dhidi ya Mukwavinyika.

Vilevile, Mukwavinyika alipigana vita na Mwambambe. Ikumbukwe kuwa, hapo awali, Mwambambe hakuwa mtawala katika jamii ya Wahehe bali alipata uongozi baada ya kufanya mapinduzi ya kumpindua Mukwavinyika. Utawala wa Mwambambe ulikuwa ni utawala wa kikatili ambao Wahehe waliupinga na kuukataa. Kutokana na hayo, Wahehe walifanya shauri la siri kumuomba Mukwavinyika arudi kuja kupigana vita na Mwambambe. Hayo yameelezwa katika kisakale hicho kama ilivyonukuliwa katika data namba (2).

(2) ...Aliporudi Uheheni, Mukwavinyika hakukawia kusimamisha jeshi la Wahehe waaminifu kisha akamshambulia Mwambambe pande zote na kumsukuma mbele mpaka Usawila. Katika mapigano makali sana, Mwambambe akashindwa na akawa hana budi zaidi ya kukimbilia nchi nyingine. Mwambambe alichagua kukimbilia Kiwere katika Ukimbu...

Kama ilivyokuwa kwa Wangoni, Mukwavinyika pia alifanikiwa kumpiga vita Mwambambe mpaka Mwambambe akakimbia kwenda kuishi katika nchi nyingine.

Sio hivyo tu bali pia, Mukwavinyika alipigana vita vya utetezi mara kadhaa na Wajerumani ambao walikuwa wamekuja kuivamia Tanganyika. Katika kisakale hicho imeelezwa kama ilivyonukuliwa katika data namba (3).

(3) ...Mkuu wa kikosi cha Kijerumani aliitwa Kamanda Emil Von Zelewski aliongoza jeshi lake huyoooo! kupigana vita na jeshi la Mukwavinyika. Katika mapigano hayo kiongozi wa Wajerumani aliuawa pamoja na askari wake wengi ambao walitapakaa chini mithili ya kumbikumbi...

Maelezo hayo katika data namba (3) yanathibitisha kuwa Mukwavinyika alikuwa na nguvu za kivita kwa sababu alipigana vita na Wajerumani. Ikumbukwe kuwa Wajerumani walikuwa ni taifa lenye nguvu ambalo lilitumia silaha za moto kama vile bunduki. Hata hivyo, Mukwavinyika alitumia silaha za jadi ambazo ni mishale na mikuki. Katika vita hiyo, Mukwavinyika aliwaua askari wengi wa Kijerumani kisha akachukua silaha zao na kuzihifadhi katika ngome yake huko Kalenga. Kwa ujumla, imebainika kuwa Mukwavinyika alikuwa mzalendo na mkombozi wa wanajamii kutokana na vita vya utetezi alivyopigana kwa ajili ya jamii yake.

**Umoja na Mshikamano**

Sio hivyo tu, bali pia dhamira ya umoja na mshikamano imeibuliwa na sifa ya shujaa kuungwa mkono na wanajamii. Mawazo ya wafuasi wa Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika yanaeleza kuwa shujaa lazima aungwe mkono na wanajamii kwa sababu shujaa huanguka pindi asipoungwa mkono na wanajamii (Kazinja, 2017; Mulokozi, 2017 na Sosoo, 2018). Hivyo basi, mashujaa wanapata wafuasi wa kuwaunga mkono kutokana na umoja na mshikamano walionao na wanajamii. Shujaa asipokuwa na umoja na wanajamii hataweza kufanikiwa kutatua matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii. Katika kisakale cha "Mukwavinyika" imebainika kuwa Mukwavinyika aliungana na baadhi ya Wahehe katika vita vya aina mbili. Mosi, Mukwavinyika aliungana na Wahehe kwa ajili ya kumtoa Mwambambe madarakani (Rejea data namba 2). Vilevile, Mukwavinyika aliungana na Wahehe katika vita vya utetezi dhidi ya Wajerumani (Rejea data namba 3). Katika mapigano ya mara ya kwanza Mukwavinyika na wafuasi wake walishinda baada ya kufanikiwa kumtoa Mwambambe madarakani. Ushindi huo unadhihirisha ni kwa jinsi gani nguvu ya umoja kati ya Wahehe na Mukwavinyika ilivyosaidia kumfukuza Mwambambe. Hii, inadhihirisha kwamba, bila ya kuwa na umoja Wahehe wasingeweza kumtoa Mwambambe madarakani kwa sababu Mwambambe alikuwa ni mtu mwenye nguvu na mbabe. Pia, hata katika mapigano ya mara ya pili jeshi la Wahehe kwa umoja wao walifanikiwa kuwashinda Wajerumani katika vita.

**Imani ya Uchawi na Ushirikina**

Mbali na hayo, katika kisakale cha "Mukwavinyika" dhamira ya imani ya uchawi na ushirikina imeibuliwa na sifa ya shujaa kuongozwa na nguvu za kichawi na kimiujiza. Wafuasi wa Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika wanaamini kuwa mashujaa wa Kiafrika huongozwa na nguvu za sihiri, uchawi na ushirikina (Mulokozi, 2017 na Mpalanzi, 2019). Akifafanua mawazo hayo, Mpalanzi (2019) anaeleza kuwa sihiri ni nguvu ya ziada ambayo shujaa anaipata kutoka katika vyanzo vya aina mbalimbali kama uganga na mizimu. Vilevile, Mpalanzi anafafanua kuwa uchawi ni ufundi wa kutumia dawa au vitabu maalumu vya uganga ili kuleta madhara kwa viumbe. Kutokana na hayo, uchawi hutokea pale mtu anapotumia nguvu za kimiujiza kwa lengo la kumdhuru mtu. Hata hivyo, Mulokozi (2017) anaeleza kuwa uchawi unaweza kushindwa na uchawi wenye nguvu zaidi. Suala la shujaa kutumia nguvu za kichawi na kimiujiza limejitokeza katika kisakale cha "Mukwavinyika". Katika kisakale hicho, imeelezwa kuwa, Mukwavinyika alitumia dawa kwa ajili ya kuwagundua wabaya wake na katika kumbaini mke wake anayetaka kusaliti ndoa. Hayo, yameelezwa kama yalivyonukuliwa katika data namba (4).

> (4) ...Mukwavinyika alikuwa anatumia dawa za kienyeji kutoka kwa mganga ambazo alikuwa anaziweka katika dira ili zimuoneshe mwanamke anayetaka kusaliti ndoa. Kwa msaada wa dawa aliwagundua wake zake wawili wasaliti na akawapa adhabu ya kuwakata masikio...

Maelezo hayo katika data namba (4) yanathibitishia kuwa Mukwavinyika alitegemea sana nguvu za kichawi na kimiujiza katika kutatua matatizo mbalimbali. Matumizi ya dawa hizo yalimfanya Mukwavinyika kuogopeka na wanajamii kwa sababu alikuwa na nguvu nyingi.

**Uzazi**

Pia, dhamira ya uzazi imeibuliwa na sifa ya shujaa kuwa lazima awe rijali. Sifa hii ni mojawapo ya mawazo ya wafuasi wa Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika kuwa ili mtu awe shujaa lazima awe rijali (Mahenge, 2016; Mulokozi, 2017 na Sosoo, 2018). Kwa mfano, Mulokozi (2017) anaeleza kuwa urijali kwa undani wake unahusu suala la uzazi kama kigezo muhimu cha ushujaa, utajiri na umilele katika Ontolojia ya Kiafrika. Kutokana na hayo, ili shujaa awe rijali ni lazima awe na uwezo wa kuzaa watoto kwa sababu hata kama atafariki atakuwa anaendelea kuishi kutokana na watoto wake. Hivyo basi, kitendo cha shujaa kuzaa watoto ndicho kinachotimiza dhana ya umilele kwa Mwafrika kwa sababu mtu atakumbukwa kutokana na watoto wake aliowaacha duniani. Suala hili la shujaa kuwa rijali limejitokeza katika kisakale cha "Mukwavinyika." Katika kisakale hicho imebainika kuwa Mukwavinyika alioa wanawake sitini na mbili ambao alizaa nao watoto wengi. Hoja hii imefafanuliwa kama ilivyonukuliwa katika data namba (5).

(5) ...Mukwavinyika alikuwa na wake sitini na mbili. Mtawala huyu kila mwanamke mzuri aliyekuwa anamuona alitaka awe mke wake. Katika idadi ya wake zake ni wachache tu wajulikanao na watoto wao...

Maelezo katika data namba (5) yanaonesha kuwa Mukwavinyika alikuwa rijali kwa sababu alizaa watoto kwa wanawake aliowaoa. Hivyo, kutokana na hayo, inathibitika ni kwa jinsi gani Waafrika wanathamini sana uzazi kwa sababu wanaona uzazi ni njia ya uzima wa milele. Ingawa Mukwavinyika alifariki lakini alikuwa anakumbukwa kwa sababu aliacha watoto wake ambao walirithi utawala wake.

**Kifo**

Dhamira hii imeibuliwa na sifa ya shujaa kujiumbia jaala yake. Wafuasi wa Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika wanaeleza kuwa, shujaa huwa anasaka au anafuata jaala yake (Mulokozi, 2017 na Kazinja, 2017). Katika jamii za jadi za Kiafrika, Waafrika wanaamini kuwa kila mtu ana majaaliwa yake ambayo huenda akayapata kwa kuyatafuta mwenyewe au yakawa yamepangwa na Mungu. Katika kisakale cha "Mukwavinyika" imebainika kuwa shujaa huyu anajiumbia jaala yake ambayo ni kifo. Mukwavinyika alijiumbia jaala yake mwenyewe baada ya kujipiga risasi ili asikamatwe na Wajerumani. Katika kisakale hicho imeelezwa kuwa Mukwavinyika alipoona anakaribia kukamatwa na Wajerumani alijipiga risasi kisha akafariki. Hili limethibitika kama lilivyonukuliwa katika data namba (6).

(6) ...Mkwawa alipoona Mwasamila amewahi kurudi na kishaijua siri yake kuwa anataka kujiua alianza kwanza kummiminia risasi Mwasamila kama mvua na kisha akajiua na yeye mwenyewe puuuuuu! ...

Kitendo cha Mukwavinyika kujiua kimemfanya shujaa huyu kuifikia jaala yake kwa njia ya kujiumbia yeye mwenyewe na si kwa njia ya kuisaka wala kuifuata. Mukwavinyika alijiumbia jaala yake kwa sababu hakuna utabiri wowote ambao ulitabiriwa na miungu kuwa Mukwavinyika atajiua mwenyewe. Hivyo, tunaona jinsi dhamira ya kifo ilivyoibuliwa vizuri na sifa ya shujaa kujiumbia jaala yake.

**Imani Juu ya Wahenga na Mahoka**

Mbali na hayo, dhamira ya kuamini wahenga na mahoka imeibuliwa na sifa ya shujaa kusaidiwa na wahenga au mahoka. Wafuasi wa Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika wanaeleza kuwa, shujaa wa Kiafrika lazima asaidiwe na wahenga au mahoka (Mahenge, 2016; Mulokozi, 2017 na Sosoo, 2018). Wahenga hao hukumbukwa kwa njia mbalimbali mfano kwa kutajwa majina, kutambikiwa na kuombwa msaada wa kutatua matatizo mbalimbali. Hivyo basi, kwa Waafrika wahenga bado wanaendelea kuishi hata kama wameshafariki dunia. Suala hili ndilo linalowafanya Waafrika kuamini kuwa kifo sio mwisho wa uhai bali ni mwanzo wa maisha mengine (Tempels, 1959). Katika kisakale cha "Mukwavinyika" imebainika kuwa Mukwavinytika alisaidiwa na wahenga kutatua tatizo lilomkabili. Katika kisakale hicho imeelezwa kwamba, Mukwavinyika alitokewa kwenye ndoto na

baba yake mzazi ambaye alimueleza mbinu za kumuua Mwambambe. Naye, alimueleza kwamba ili Mwambambe afe inabidi achomwe mkuki katika dole gumba na kwenye kisigino. Baada ya kufahamu mbinu hiyo, mfuasi wa Mukwavinyika ambaye ni Mkimayena alimchoma Mwambambe mkuki kama ilivyoelekezwa ndipo Mwambambe akakata roho. Suala hili limeelezwa katika kisakale hicho kama ilivyonukuliwa katika data namba (7).

(7) ...Munyigumba alimueleza Mukwavinyika mbinu za kumuua Mutwa Mwambambe. Alimweleza kuwa "ili Mwambambe afe, anatakiwa achomwe mkuki katika dole gumba au kwenye kisigino." Baada ya kuijua mbinu hiyo, Mukwavinyika alimwambia Mkimayena amchome mkuki Mwambambe kama ilivyoelekezwa. Mkimayena alimchoma mkuki Mwambambe kwenye dole gumba na kwenye kisigino na hapohapo Mwambambe alianza kuhisi kichefuchefu lakini inaonekana mkuki huo haukumwingia sana. Askari mwingine wa Mukwavinyika ambaye ni Mwakapanzi alitupa mkuki ambao ulimpata Mwambambe mpaka ukatokeza upande wa mgongo. Watu walioshuhudia walimuona Mwambambe anaishiwa nguvu na kuanguka chini puuuuuuuuuu! kama gunia. Baada ya Mwambambe kukata roho, wafuasi wa Mukwavinyika walifurahi na walikula maiti ya Mwambambe kisha wakailamba damu iliyokuwapo kwenye mchanga huku wakiwa na imani kuwa nguvu alizokuwanazo Mwambambe zitawaingia wao...

Maelezo katika data namba (7) yanaonesha jinsi shujaa Mukwavinyika alivyopata msaada wa kumuua Mwambambe kutoka kwa wahenga. Mwambambe alikuwa ameuzindika mwili wake kwa kutumia dawa ili asidhurike kwa kitu chochote. Hata watu walikuwa wanamshangaa Mwambambe kwa sababu alikuwa na nguvu nyingi za ajabu ambazo alizipata kutokana na zindiko alilojizindika. Hivyo basi, Mwambambe aliuawa na Mukwavinyika baada ya zindiko la sihiri yake kugundulika.

**Matabaka**

Dhamira hii imeibuliwa kutokana na sifa ya shujaa inayoeleza kuwa shujaa wa Kiafrika hutoka katika tabaka lolote. Wafuasi wa Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika wanaeleza kuwa, shujaa wa Kiafrika anaweza kutoka katika tabaka la juu au la chini (Mahenge, 2016; Mulokozi, 2017; Kazinja 2017 na Sosoo, 2018). Masuala haya pia yamejibainisha katika kisakale cha "Mukwavinyika." Katika kisakale hicho imebainika kuwa Mukwavinyika alikuwa ni mtoto wa mtawala ambaye alitawala katika jamii ya Wahehe. Hayo yameelezwa kama ifuatavyo:

(8) ...Baba wa Mukwavinyika alivamiwa na Wangoni katika utawala wake na aliokolewa na mtoto wake ambaye ni Mukwavinyika. Baada ya kuokolewa na mtoto wake, alifurahi huku akijisifu kuwa hakuna mtu wa kumshinda katika vita. Mara tu baada ya kumaliza vita hivyo Mukwavinyika alipewa jina hilo na baba yake kutokana na uhodari wake wa kivita.

Hii inaonesha kuwa, baba yake Mukwavnyika alikuwa ni mtawala katika jamii ya Wahehe. Hivyo basi, Mukwavinyika anatoka katika tabaka la juu kwa sababu alikuwa ni mtoto wa mtawala wa jamii ya Wahehe.

**Usaliti**

Dhamira hii imeibuliwa na sifa ya shujaa kusalitiwa na watu wake wa karibu. Wafuasi wa Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika wanaelekea kuamini kuwa mara nyingi shujaa husalitiwa na watu wake wa karibu (Mulokozi, 2002; Lyamuya, 2014 na Sosoo, 2018). Katika kisakale cha "Mukwavinyika" imebainika kuwa Mukwavinyika alisalitiwa na watu wake wa karibu ambao ni Mbogamasoli na Msatima. Katika kisakale hicho imeelezwa kuwa, Mukwavinyika alisalitiwa na ndugu zake wa karibu wakati wa mapambano dhidi ya Wajerumani. Suala hili limeelezwa katika kisakale hicho kama ilivyonukuliwa katika data namba (9).

(9) ...Msatima alipopata habari juu ya kifo cha kaka yake Mbogamasoli alikimbilia Kilimatinde kwa shangazi yake kwa sababu alihofu naye angeuwawa. Alipokuwa njiani Msatima alikamatwa na jeshi la Wajerumani. Msatima alipokamatwa na Wajerumani alitoa siri zote za Mukwavinyika...

Dondoo hili linaonesha kuwa Mukwavinyika alishindwa katika mapambano ya mara ya pili na Wajerumani kwa sababu alisalitiwa. Hata hivyo, Mukwavinyika alipofanya upelelezi aligundua kuwa Mbogamasoli ndio alikuwa mtu wa kwanza kutoa taarifa kwa Wajerumani na alimpa adhabu ya kifo. Vilevile, mdogo wa Mbogamasoli aitwaye Msatima baada ya kusikia kuwa kaka yake ameuliwa na Mukwavinyika hakurudi Kalenga kwa sababu aliogopa na yeye atauawa. Hata hivyo, Msatima alipokuwa njiani alikamatwa na Wajerumani na wakamuambia ili awe huru awaeleze habari zote za Mukwavinyika. Msatima aliwaambia Wajerumani habari zote za Mukwavinyika kisha Wajerumani walimvamia Mukwavinyika kwa mara ya pili.

**Nafasi ya Mwanamke katika Jamii**

Sio hivyo tu, bali pia imebainika kuwa dhamira ya nafasi ya mwanamke imeibuliwa na sifa ya shujaa kumpa mwanamke nafasi muhimu katika ushujaa. Wafuasi wa Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika wanaonekana kuamini kuwa, ushujaa ni sifa inayohusiana na uanaume. Wananadharia hao, wanaamini kuwa, mashujaa wote ni wanaume na kwamba ushujaa ni sifa inayofungamana na uanaume (Johnson, 1986; Mulokozi 1999 na Gathara 2015). Ingawa katika miaka ya hivi karibuni kumeibuka wananadharia wanaojaribu kuonesha kuwa kuna mashujaa wa kike (Samwel, 2012; Sungi, 2011 na Kazinja, 2017). Katika kisakale cha "Mukwavinyika" imebainika kuwa mwanamke kama ilivyo kwa mwanaume amehusishwa katika masuala muhimu ya kishujaa. Katika kisakale hicho imeelezwa kuwa Mukwavinyika alimpa nafasi ya uongozi katika kikosi cha kivita mwanamke aitwaye Mtage. Katika kisakale hicho imeelezwa kama ilivyonukuliwa katika data namba (10).

(10) ...Mbogamasoli alikuwa kwenye kikosi kilichoongozwa na Mwanamke aitwaye Mtage...

Maelezo katika data namba (10) yanaonesha jinsi shujaa Mukwavinyika alivyomthamini mwanawake kwa sababu alimpa nafasi ya juu ya uongozi katika kikosi cha kivita. Jamii mbalimbali za Kiafrika zinamthamini mwanamke katika masuala mbalimbali kama vile masuala ya elimu na hata uongozi. Hivyo basi, tunaona jinsi shujaa Mukwavinyika ambavyo alivyomthamini na kumwamini mwanamke kuwa anaweza kuwa kiongozi jasiri. Mwanamke katika uongozi wa Mukwavinyika alipewa nafasi ya kuwa kiongozi katika kikosi cha kivita ambayo ilikuwa ni nafasi ya juu sana katika uongozi.

**Motifu**

Wamitila (2003) anaeleza kuwa, motifu hutumiwa kurejelea wazo kuu na sehemu ya dhamira katika kazi ya fasihi. Wamitila anaeleza zaidi kuwa motifu huweza pia kuelezea elementi ya kimuundo au kimaudhui inayotawala kazi fulani. Naye, Mulokozi (2017) anaeleza kuwa motifu ni kipengele radidi cha kijadi au kikaida au kimaudhui kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao ili kutoa ujumbe fulani. Kutokana na hayo, motifu hujitokeza kama kipengele cha kimaudhui na kifani kinachosaidia kutoa ujumbe fulani wa kazi ya fasihi. Katika kisakale cha "Mukwavinyika" zimejitokeza motifu za aina mbili ambazo ni motifu ya mnyonge kumshinda mwenye nguvu na motifu ya safari. Motifu hizo zimefafanuliwa kama ifuatavyo:

**Motifu ya Mnyonge Kumshinda Mwenye Nguvu**

Motifu ya Mnyonge kumshinda mwenye nguvu imeonekana kutawala na kuwa kiungo kikubwa cha matukio katika kisakale cha "Mukwavinyika" hasa katika suala la kudhihirisha ushujaa. Mukwavinyika alipigana vita na Mwambambe ambaye alikuwa anasifika sana kuwa ni jitu katili na lenye nguvu sana. Hata hivyo, Mukwavinyika alipigana vita na Mwambambe na akashinda (Rejea data namba 2). Pia, Mukwavinyika alipigana vita na Wakoloni wa Kijerumani ambao walikuwa ni wakoloni wenye nguvu hasa za kivita na alishinda vita katika awamu ya kwanza (rejea data namba 3). Matukio haya ya Mukwavinyika kushinda katika mapigano ambayo yalihusisha watu wenye nguvu kama Mwambambe na Wajerumani yamekuwa ni kiungo kikuu katika harakati zake za kudhihirisha ushujaa.

**Motifu ya Safari**

Motifu ya safari ni aina ya motifu iliyojitokeza katika kisakale cha "Mukwavinyika." Katika kisakale hicho imeelezwa kuwa Mukwavinyika alisafiri kutoka Uheheni kwenda kuishi kwa mjomba wake huko Dodoma. Sababu ya Mukwavinyika kusafiri ni baada ya kupinduliwa madarakani na Mwambambe. Hivyo, Mukwavinyika alisafiri kwa kuogopa asije akauliwa na Mwambambe. Hayo yameelezwa katika kisakale hicho kama ilivyonukuliwa katika data namba (11).

(11) ...Mukwavinyika alipokuwa anatoroka Ng'uluhe, alijipaka udongo mwekundu usoni kisha akajifunika nguo mwili mzima ili apate kupita katika nchi ya Uhehe bila kugundulika. Hatimaye, Mukwavinyika alifanikiwa kupita nchi ya Uhehe akaelekea katika nchi ya Ugogo...

Pia, Mukwavinyika alisafiri tena kurudi Uheheni kwa lengo la kupigana vita na Mwambambe ili kumtoa Mwambambe madarakani (Rejea data namba 2). Vilevile, Mukwavinyika alifukuzwa tena na Wajerumani katika utawala wake na akasafiri kutoka Kalenga kwenda kuishi Mulambalasi. Hata hivyo, Mukwavinyika alipoishi Mulambalasi ndio ukawa mwisho wa maisha yake kwa sababu alikufa kwa kujipiga risasi (Rejea data namba 6). Kutokana na hayo, inaonesha jinsi maisha ya Mukwavinyika yalivyotawaliwa na safari.

**Falsafa ya Maisha**

Falsafa ya maisha ni mojawapo ya kipengele cha kimaudhui kilichojitokeza katika kisakale cha "Mukwavinyika." Mukwavinyika anaonekana kuathiriwa na falsafa ya maisha ya jamii za Kiafrika kwa kuona kuwa maisha haya hayana maana ila kuna maisha baada ya kifo. Tempels (1959) anaeleza kuwa Waafrika wanaamini kifo sio mwisho wa uhai bali ni mwanzo wa kuanza kuishi maisha mengine. Katika kisakale cha "Mukwavinyika" imeelezwa kuwa Mukwavinyika alipoona anakaribia kukamatwa na Wajerumani alijiua kwa kujipiga risasi (Rejea data namba 6). Mukwavinyika alijiua kwa sababu aliona heri kufa kuliko kupata fedheha duniani baada ya kukamatwa na Wajerumani. Hivyo basi, Waafrika hawaogopi kifo kwa sababu wanaona kifo ni njia ya kuanza kuishi maisha mengine.

**Hitimisho**

Makala hii, imebaini kuwa, Mukwavinyika alikuwa shujaa kwa sababu amekidhi sifa za shujaa wa Kiafrika kama zilivyopendekezwa na wafuasi wa Nadharia ya Sifa za Shujaa wa Kiafrika. Pia, makala hii imeonesha nafasi ya nduni za shujaa katika kuibua maudhui yaliyowasilishwa kupitia kazi ya fasihi. Vilevile, Makala hii imebaini kuwa nduni za shujaa zina mchango mkubwa katika kuibua maudhui yaliyowasilishwa kupitia kazi ya fasihi. Maudhui hayo ni kama vile dhamira mbalimbali, motifu na falsafa. Mbali na hayo, makala hii imeonesha ufungamano uliopo baina ya visakale na mashujaa.

**Marejeleo**

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Clarendon: Oxford University Press.

Gathara, F. (2015). Taswira ya Jagina katika Utendi: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Nabii Isa. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.

Johnson, J. (1978). The Epic of Sunjata: An Attempt to Define the Model for African Epic Poetry. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Bloomington: Chuo Kikuu cha India.

______. (1986). *The Epic of Son-Jara*. Bloomington: Indiana University Press.

Kazinja, G. (2017). Shujaa Mwanaume na Mwanamke katika Utendi: Uchambuzi wa utendi wa *Rasi'lGhuli* na utendi simulizi wa *Kachwenyanja*. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lyamuya, H.N. (2014). "Ulinganishi wa Sababu za Kuanguka kwa Shujaa katika Utendi wa Kiswahili na Tendi Nyingine za Kiafrika." Tasinifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mahenge, O. (2016). Shujaa wa Jamii ya Wakinga. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mlaga, K. W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishera Ltd.

Mpalanzi, L. (2019). Ujitokezaji wa Falsafa ya Kiafrika katika Riwaya za Kiethnografia za Kiswahili. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mtega, W. (2017). Uhusiano wa Taashira na Maisha ya Shujaa wa Kiutendi: Uchunguzi wa Utenzi wa Rasi'lGhuli na utenzi wa Nyakiiru Kibi. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (Mh) (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.

______. (2002). *The African Epic Controversy*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publisher.

______. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Ngule, A. (2003). *Fasihi Simulizi*. Nairobi: Phoenix Publishers

Okpewho, I. (1979). *The Epic in Africa: Towards a Poetics of the Oral Performance*. London: Longman.

Samwel, M. (2012). *Hadithi Fupi: Nadharia, Mbinu na Mifano*. Iringa: Kasenyenda Tanzania.

Sosoo, F. (2018). Ushujaa katika Motifu ya Safari na Msako: Ulinganishi wa Ngano za Kiewe kutoka Ghana na Riwaya za Shaaban Robert kutoka Tanzania. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sungi, N. A. (2011). Ruwaza ya Shujaa Mwanamke wa Kiutendi katika Jamii ya Wanyanyembe wa Tabora. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Tempels, P. (1959). *Bantu Philosopy:* Paris: Presence Africaine.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.